**SHULE YA SEKONDARI YA KINOLE,**
**S.L.P 6487,**
**MOROGORO,**
**0718191989**
**TAREHE: 10.12.2020**

**JINA LA MWANAFUNZI: ............................**
**S.L.P 1880,**
**MOROGORO.**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KINOLE**

1. **UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya kinole iliyopo kata ya Kinole wilaya ya Morogoro mkoani Morogoro mwaka 2021. ~~Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **11/01/2021** hadi~~ **25/01/2021.**

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

a) **SARE ZA SHULE**

**WASICHANA**

*i. Sare ya shule hii ni shati 2 nyeupe mikono mifupi na Sketi 2 rangi ya zambarau*
*ii. maelezo ya mshono rinda boksi kwa wasichana na inayovuka magoti*
*iii. Hijabu inayoruhusiwa ni nyeupe isiyokuwa na maua au urembo wowote na yenye kufunika kifua*
*iv. sare za michezo kwa shule hii ni fulana yangi ya bluu bahari na traki suti za rangi ya bluu bahari*
*v. sweta rangi ya zambarau*
*vi. T-shirt rangi ya kijivu (gray) yenye nembo ya shule na itavaliwa siku za jumatano na ijumaa tu*

**WAVULANA**

*i. Sare ya shule hii ni shati 2 nyeupe mikono mifupi na suruali 2 rangi ya zambarau Maelezo ya mshono suruali iwe na marinda mawili na mkunjo chini (turn up) isiyobana*
*ii. sweta rangi ya zambarau*
*iii. T-shirt rangi ya kijivu (gray) yenye nembo ya shule na itavaliwa siku za jumatano na ijumaa tu*

**iv. MAHITAJI MENGINE**

a. viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba kwa wote visiwe na visigino virefu
b. soksi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
c. tunasisitiza sketi ndefu inayovuka magoti, pia
d. tunasisitiza suruali isibane na iwe na mkunjo chini (Turn up)
e. Daftari (counter book Q3) tisa (9) kwa wote na mkebe kwa ajili ya masomo ya sayansi
f. mkanda mweusi kwa wavulana
g. raba nyeupe kwa ajili ya michezo kwa wote
**h. meza na kiti**

**v. VIFAA VYA USAFI**

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na fagio moja ( chelewa) na ndoo moja ndogo
ii. fyekeo moja (kwanja/panga) kwa wavulana
iii. jembe moja lenye mpini kwa wasichana

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni ( preparation) .
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na zingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wq mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule kwa wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule;**

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji, ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
8. Kudharau bendera ya shule
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama shule au watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kutoroka shule wakati ratiba za masomo zikiendelea.

Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

i. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
ii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

**Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA KINOLE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KINOLE
S.L.P. 6487, MOROGORO

**RASHIDI A GUGU**
**MKUU WA SHULE**

**SEHEMU A** (ijazwe na mzazi/ mlezi)
Mimi ........................................... mzazi/ mlezi wa mwanafunzi....................................
Ninaahidi kwamba nitamtunza kijana wangu ambaye ni.............................................kwa kipindi chote cha masomo yake atakapokuwa shuleni na kuhakikisha kwamba mwanangu atatii na kuziheshimu sheria zote zilizowekwa shuleni vilevile nitamtekelezea mahitaji yake yote muhimu ili aweze kuendelea na masomo yake.

Sahihi ya mazizi/ mlezi.......................................
Jina la mzazi/mlezi...............................................

**SEHEMU B** (ijazwe na mwanafunzi)
Mimi ... dini yangu ni............................. Shule ninayotoka .............................. jina la mzazi/mlezi wa kiume ni ............................................ na mzazi wa kike ni ........................................... nikiwa kama mwanafunzi wa shule ya sekondari ya kinole, ninaahidi kuwa nitazitii na kuziheshimu sheria zote za shule.

Sahihi ya mwanafunzi.............................................
Jina la mwanafunzi: ...........................................

***fomu hii irudishwe pindi mwanafunzi anaporipoti shuleni**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

THE HEADMASTER/MISTRESS,
KINOLE SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 6487,
MOROGORO.

TO BE FILLED BY MEDICAL OFFICER IN RESPECT OF ALL FORM ONE ENTRANTS AND NEW SCHOOL EMPLOYEES

PUPIL'S NAME: ………………………………………………………………

AGE ........................................................... ( YEARS)

BLOOD COUNT ( RED AND WHITE) ……………………………………………………

STOOL EXAMINATION …………………………………………………………………

URINE ANALYSIS ………………………………………………………………………

SYPHILIS TEST …………………………………………………………………………..

T.B TEST ……………………………………………………………………………......

EARS ………………………………………………………………………………………

CHEST ……………………………………………………………………………………

ABDOMEN ……………………………………………………………………………..

SPLEEN …………………………………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION

E.g physical defects or impairments, infects chronic of family diseases Etc.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

I certify that above is fit/unfit for admission into a day/boarding school

Signature ……………………………………………. designation ……………………………………..

Station ……………………………………………………………………………………………………

Date ………………………………………………………………………………………………………

Note: medical officer at the time of examination please treat the individual for any illness you note. This complete form should be sent to the head of school.

No pupil or person may be enrolled without certification of physical fitness.